

جمعية الدعوة والإرشاد وتنمية الجاليات بالزلفي

مشروع تعلم الإسلام – أصول العقيدة - سواحيلي

Samo la 8

الدرس الثامن

6- Ikhlas nayo ni kutakasa mwanadamu matendo yake mema kwa nia njema , kutokana na chembechembe za kishirikina, kwa kufanya matendo yake yote ya maneno au ya vitendo yawe ni kwa ajili ya Allah (sw) na kutafuta radhi zake Allah, asiyafanye kwa kujionyesha kwa watu, au asemwe, au anafanya kwa kutaka manufaa fulani, au lengo maalumu, au anafanya kwa matamano yaliyowazi au yaliyojificha, au anamkingia mtu kwa ajili ya mapenzi, madhehebu, kundi lisilokuwa kwenye muongozo wa Allah (sw), bali hapana budi yote atakayoyafanya ayafanye kwa kutafuta radhi zake Allah (sw) na malipo kesho Akhera, hatafuti kulipo na mtu yejote wala kushukuriwa na mtu.

قال الله تعالى: ﴿أَلَا لِلَّهِ الدِّينُ الْحَالِصُ﴾ [الزمر: ٣]

Allah (sw) anasema : (" Juwa na kutambua ya kuwa Allah peke yake ndie mwenye dini iliyotakasika") (Az-Zumar: 3).

وقال سبحانه: ﴿وَمَا أُمْرُوا إِلَّا لَيَبْدُوا اللَّهَ مُحْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ﴾ [آلـبيتـة: ٥]

Anasema Allah (sw) : (" Na hawakuamrishwa katika sharia zote zilizopita isipokuwa ni wamuabudu mwenyezi mungu peke yake, hali ya kutakasia yeye dini") (Al-Bayyinah:5).

Na imekuja kwenye sahihi mbili, bwana Mtume (saw) anasema :

وفي الصحيحين من حديث عتبان قوله عليه السلام: «فَإِنَّ اللَّهَ قَدْ حَرَمَ عَلَى النَّارِ مَنْ قَالَ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، يَبْتَغِي بِذَلِكَ وَجْهَ اللَّهِ» [متفق]

عليه السلام: [٤٢٥، ٤٣٣].

("Hakika ya Allah (sw) ameharamisha moto kuunguza mwenye kusema LAAILAHA ILLALLAH akitafuta radhi za Allah") (Ameipokea Bukhar na Muslim).

7- Kupenda, nako ni kuipenda LAAILAHA ILLALLAH na kila ambacho kinafungamana na hili neno, na ampende Allah na Mtume wake, na atangulize mapenzi ya kumpenda Allah na Mtume wake kulikoni kitu chochote kile, ampende Allah mapenzi yanayo fungamana na utukufu wake Allah, na ukubwa wake Allah, na khofu yake Allah, na atarajie mema kutoka kwake Allah, na azipende sehemu zote anazozipenda Allah (sw) kama vile Makka, Madina na misikiti yote iliyopo duniani, na azipende zama kama vile mwezi wa Ramadhan, masiku kumi ya mwezi wa Dhul Hijja na masiku mwengine, na awapende viumbe watukufu kama vile Manabii, Mitume, Malaika wote, waja wema, Mashahidi, na pia apende matendo mema kama vile Swala, Zakat, Swaumu, Hijjah, na pia apende dhikri za kumtaja Allah na apende kusoma Quran.

Na mionganini mwa mapenzi kwa Allah ni kutakunguliza kila aina ya mapenzi kwake Allah kulikoni mapenzi ya nafsi yake mtu pamoja na matamaniwa yake.

Pia achukie kila ambacho Allah anakichukia, achukie ukafiri, ufasiki na uovu.

Allah (sw) anasema :

قال الله تعالى: ﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا مَنْ يَرْتَدَّ مِنْكُمْ عَنِ دِينِهِ فَسَوْفَ يَأْتِي اللَّهُ بِقَوْمٍ يُجْهِبُهُمْ وَيُجْهِبُونَهُ أَذْلَهُ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ أَعْزَهُ عَلَى الْكَافِرِينَ يُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلَا يَخَافُونَ لَوْمَةَ لَا إِيمَانٍ﴾ [آلـمـائـة: ٥٤]

("Enyi mliaoamini, yoyote kati yenu atakayerudi nyuma akaiacha dini yake, basi Allah atawaleta watu bora kuliko wao, anao wapenda na wanompenda, mwenye huruma kwa waumini, wakali kwa makafiri, wanapigana jihadi na maadui wa mwenyezi mungu, na hawaogopi lawama za mwenye kulaumu") (Al-maidah:54).